Leo ni siku ya pekee sana kwa Kanisa Katoliki Tanzania na hususan Jimbo la Iringa, ambapo tumejaliwa kushiriki matukio mawili makubwa na muhimu. Kwanza, kumbukumbu ya miaka 125 tangu tulipopokea imani ya Kikristu katika jimbo letu mwaka 1898 na Pili, kumbukumbu ya miaka 50 tangu Mhashamu Baba Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa alipopewa daraja takatifu la upadre. Kwa sababu hiyo naomba tuungane kumshukuru Mungu kwa makofi, vigelegele, vifijo na nderemo.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Naomba kuleta kwako Mhashamu Baba Askofu Ngalalekumtwa na Kanisa zima, salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jubilei hii ya miaka 125 ya Ukristu Jimboni Iringa na miaka 50 ya ukuhani wako. Mhashamu Baba Askofu, Mheshimiwa Rais anakuombea afya njema, utumishi mwema na maisha marefu. Aidha, anakusihi wewe na wakleri wote kuendelea kuliombea Taifa letu na kuwaongoza waamini kudumisha samani na umoja. Aidha, amesisitiza kwamba sisi sote yatupasa tujifunze kutoka kwako Baba Askofu, uvumilivu, unyenyekevu, kuchukuliana, kujitoa sadaka kwa ajili ya wengine na kutekeleza vema wajibu wetu kwa Mungu na Taifa.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Kwa namna ya pekee napenda tuungane pamoja kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka na neema alizomjalia mtumishi wake Mhashamu Baba Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa. Hakika, neno la Mungu limekuwa ndiyo taa yake katika miaka yote 50 ya ukuhani wake. Kwa kupitia kwake, sisi wana Iringa tumepokea neema na baraka hizo ambazo Mhashamu Baba Askofu ametushirikisha kwa njia ya mafundisho na maombezi yake, kama tusomavyo katika kitabu cha *2 Nyakati 30:27* kwamba ***"Ndipo wakasimama makuhani Walawi, wakawabariki watu; ikasikiwa sauti yao, sala yao ikafika hata makao yake matakatifu, yaani mbinguni."***

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Mtume Paulo katika waraka wake wa pili kwa Wakorintho *(2 Wakorintho 11:23-28)* anauelezea utumishi katika Kanisa kuwa ni zaidi katika taabu, vifungo, mapigo, hatari, masumbufu ya kukesha na kufunga mara nyingi. Ni wazi nawe Mhashamu Baba Askofu Ngalalekumtwa umepitia taabu na vikwazo vingi katika kipindi hiki cha miaka 50 ya upadre wako. Hivyo, kanisa zima tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu aliyekuwezesha kuubeba msalaba wako na tunakupongeza kwa dhati kwa kuifikia siku hii.

Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza Waamini wenzangu kusali na kuwaombea makuhani na watawa wetu ambao Mwenyezi Mungu amewatuma kwetu ili kutuongoza katika njia itupelekayo mbinguni ili kufikia lile kusudio la Mungu la kutuumba, kwamba tumjue, tumpende, tumtumikie na mwisho tufike kwake juu mbinguni, anakowashibisha watakatifu kwa uzuri wa sura yake. Aidha, tunawajibika pia kuombea miito mitakatifu ili Mwenyezi Mungu apeleke watenda kazi wengi zaidi shambani mwake. Maana tunatambua kwamba Baba Askofu Tarcisius na Makuhani wa umri wake, vichwa vinazidi kuwa vyeupe na idadi ya waamini inaongezeka.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumbukumbu hii muhimu ya miaka 125 tangu mbegu ya ukristu ilipopandwa na Wamisionari hapa kwetu Iringa. Nawaomba muungane nami kuwashukuru na kuwapongeza Wamisionari Wabenediktini (Benedictine Fathers and Sisters) ambao natumaini wawakilishi wao tunao hapa siku ya leo, kwa kazi ya uinjilishaji waliyoianzisha katika jimbo la Iringa tena katika mazingira magumu. Historia inaonesha kuwa kazi ya uinjilishaji iliyofanywa na Wamisionari wa kwanza haikuwa rahisi, kwani ilizongwa na vikwazo vingi vikiwemo kukataliwa, kuuawa na kuteseka kwa magonjwa. Nawapongeza kwa uvumilivu na kujitolea maisha yao huku wakisukumwa na upendo wa Mungu, kuhakikisha huduma za kiroho na kijamii zinawafikia wana Iringa. Tunafurahi kuona kuwa licha ya changamoto na makwazo mengi yaliyowasibu, Kanisa limezidi kustawi na kushamiri. Leo tunapoadhimisha na kumshukuru Mungu kwa miaka 125 ya uinjilishaji, tunamshukuru pia kwa ajili ya sadaka, machozi, jasho na maisha ya watu wote waliojitolea na wanaoendelea kujitolea kuhakikisha kazi ya uinjilishaji inaendelea jimboni Iringa. **Tumshangilie Mungu wetu.**

Napenda kuwahakikishia waamini wa Jimbo Katoliki la Iringa na Watanzania wote kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kanisa Katoliki katika kumwinua na kumstawisha mwanadamu kiroho na kimwili. Katika miaka 125 ya uinjilishaji, Kanisa Katoliki katika Jimbo la Iringa limekuwa likishughulikia ustawi wa jamii kwa kuwa ni jukumu la Kanisa kumkomboa mwanadamu dhidi ya dhambi na taabu zinazomsonga kimaisha. Serikali inathamini sana mchango mkubwa wa Kanisa Katoliki katika kuimarisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za jamii hususan afya na elimu. Mathalan, kwa kupitia shule maarufu ya Tosamaganga, Seminari ya Mafinga na Seminari ya Konsolata tumeweza kupata wataalam na viongozi wengi ndani na nje ya Serikali. Baadhi ya washauri wangu

(Madaktari wawili na Mwandishi wa hotuba) ambao ni ninao hapa wamepitia katika shule hizi. Aidha, kwa kupitia hospitali, zahanati na vituo vya afya vilivyokuwa vinamilikiwa au vinavyomilikiwa na Kanisa Katoliki wananchi wengi wanapata huduma muhimu za afya. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, na Serikali yake ninapongeza kwa dhati ushirikiano mzuri uliopo kati ya taasisi za dini na Serikali na ninawahakikishia kuwa, Serikali itaendelea kushirikiana na madhehebu yote ya dini nchini katika kuwaletea watanzania maendeleo na kudumisha haki na amani katika Taifa.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Ni dhahiri kwamba, mazingira yaliyokuwepo mwaka 1898 wakati wamisionari wa kwanza walipofika hapa Iringa ni tofauti na mazingira yaliyopo sasa kwa kiasi kikubwa. Katika misa hii ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa miaka 125 ya uinjilishaji jimboni Iringa na miaka 50 ya Upadre wa Mhashamu Baba Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa, ninawiwa kuwashirikisha kidogo tafakari yangu juu ya "**changamoto na fursa za uinjilishaji katika zama hizi za maendeleo ya haraka ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano"** kama ifuatavyo:

**Kwanza,** ni kuenea kwa kasi kwa mafundisho potofu na imani kali za kidini. Tunashuhudia hivi sasa wimbi la mafundisho yasiyoendana na neno la Mungu tulilopokea awali kutoka kwa wamisionari. Kutokana na mafundisho hayo, baadhi ya waamini sasa wanategemea miujiza zaidi ili kupata maendeleo badala ya kufanya kazi kwa bidii. Wakati Serikali inasisitiza watu kufanya kazi, baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakiwaelekeza waamini wao kuomba na kusubiri miujiza ili wapate mali bila kufanya kazi stahiki. Vilevile, kumekuwepo na wimbi kubwa la kuenea kwa misimamo mikali ya kidini inayosababisha watu kujitoa muhanga na kupoteza maisha yao. Hapa kwetu pia wapo 'wahubiri wa miujiza' ambao wanajilimbikizia mali binafsi kutokana na sadaka za wananchi wanyonge wenye shida au matatizo mbalimbali kama magonjwa, migogoro katika ndoa, kukosa Watoto/ajira, umasikini n.k. na wahanga wengi wa mafundisho/mahubiri hayo ni akina mama. Aidha, wamekuwepo wahubiri ambao kwa uwazi na bila kificho wamekuwa wakishabikia matendo maovu kama ya ushoga na usagaji. Vilevile, bila shaka mlisikia, hivi karibuni, kuhusu kiongozi wa kidini katika nchi jirani aliyewashawishi waamini wake kufunga hadi kufa ili wakamuone Mungu upesi! Mojawapo ya sababu za kuenea kwa kasi kwa mafundisho hayo, ni matumizi potofu ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Ninawaomba sana viongozi wangu wa dini kutumia fursa ya teknolojia ya habari na mawasiliano kukemea mafundisho potofu na kufanya uinjilishaji wa neno la Mungu la kweli.

Endeleeni kuwahimiza waamini kufanya kazi kwa bidii huku wakimuomba Mungu abariki kazi za mikono yao na akili zao.

**Pili,** ni kasi kubwa ya mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Mmomonyoko huu unashuhudiwa miongoni mwetu wazazi/walezi na hata kwa vijana na watoto wetu. Kwa bahati mbaya jamii yetu na hususan vijana wanadhani kwamba kuwa wa kisasa ni kuiga wanachokiona kwenye mitandao ambacho kinafanywa na vijana wa nchi za magharibi bila kujali utofauti wa mila na tamaduni zetu. Siku hizi, tunashuhudia kuongezeka kwa mauaji ya kikatili, kuzuka kwa vikundi vya vijana vya uhalifu kama *Panya road*, biashara ya madawa ya kulevya, unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na wanawake, ongezeko la familia za mzazi mmoja, ongezeko la watoto waliozaliwa nje ya ndoa, migogoro ya ndoa, ongezeko la talaka, migogoro ya mirathi, vitendo vya ushoga na ulawiti n.k. Kwa maoni yangu tunapoadhimisha na kumshukuru Mungu kwa miaka 125 ya uinjilishaji jimboni Iringa, Kanisa na madhehebu mengine yana jukumu kubwa la kuendelea kufundisha maadili mema katika jamii kwa nguvu na maarifa zaidi, tena bila kuchoka, la sivyo Taifa letu litaangamia. Nasi wazazi na walezi tunalo jukumu kubwa na la msingi la kuwalea watoto na vijana katika maadili mema. Akina baba tusiwaachie akina mama peke yao jukumu la kulea Watoto. Tukumbuke kuwa katika waraka wa Mtume Paulo kwa Waefeso *(Waefeso 6:4)* tunafundishwa kwamba ***"Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana".*** Natoa rai kwa waamini wote wa imani mbalimbali za kidini kuwa kielelezo kwa kuishi maisha yanayoendana na mafundisho ya imani zetu.

**Tatu,** Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Kanisa na taasisi nyingine za kidini katika kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum. Naendelea kulisihi kanisa zima kuendelea kuwasaidia wahitaji katika jamii hususan watoto yatima, watu wenye ulemavu, masikini, wajane, wafungwa na wenye shida mbalimbali. Vilevile, natoa rai kwa waamini wa dini zote kujenga tabia ya kusaidia watu wenye uhitaji katika jamii na kuepuka kujilimbikizia mali isivyo halali. Tupo ambao Mungu ametubariki na mali/uwezo zaidi lakini hatutimizi wajibu wetu wa kuwasaidia wahitaji na hata wazazi wetu! Katika Maandiko Matakatifu, Nabii Isaya anatuasa kuwa ***"Jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane."*** *(Isaya 1:17)*. Wamisionari waliotuletea imani hii, hawakuhubiri neno la Mungu tu bali walijitolea pia kuhakikisha jamii yetu inapata huduma mbalimbali za jamii

**Nne,** ni changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira. Uhai wetu katika dunia hii unakabiliwa na tishio la mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira. Zimekuwepo jitihada mbalimbali za kitaifa na kimataifa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari za uharibifu wa mazingira lakini bado hakuna matokeo ya kuridhisha. Kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Iringa ni mashahidi wa kupungua kwa kina cha maji cha Mto Ruaha mkuu na hata kutotiririsha maji kabisa katika kipindi fulani cha mwaka. Vilevile, upotevu wa misitu unaonekana katika kanda mbalimbali za nchi yetu. Aidha, hali ya uharibifu wa mazingira inaonekana katika kutoweka kwa vyanzo vya maji, utupaji wa taka ngumu, uchafuzi wa fukwe za Bahari na kadhalika.

Ninawasihi waamini na watanzania wote kutambua kuwa jitihada za Serikali katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi hazitafanikiwa kama wananchi wote hatutabadili tabia na kuchukua hatua za makusudi kulinda na kuhifadhi mazingira yetu. Rai yangu kwa viongozi wa dini na waamini wa dini zote ni kuzingatia mafundisho ya imani zetu hususan kuhusu wajibu wetu wa kuitunza vema dunia tuliyokabidhiwa na Mwenyezi Mungu. Tunasoma katika Kitabu cha Mwanzo kuwa ***"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza"*** *(Mwanzo 2:15)*.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Wageni Waalikwa na Wananchi wote;***

Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais aliyenituma kumwakilisha katika ibada hii ninawatakia waamini wa Jimbo Katoliki la Iringa, wananchi wa Iringa na wote wenye mapenzi mema, Jubilei njema ya miaka 125 ya ukristu hapa Iringa. Aidha, ninamtakia Mhashamu Baba Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa afya njema na umri mrefu ili aendelee kutubariki, kutufundisha na kutuombea na impendeze Mungu tuione Jubilei yake ya Upadre ya miaka 75!

**Tumsifu Yesu Kristu.**